**NAMBA 9: MARKO 14:1-11: YESU APAKWA MAFUTA HUKO BETHANIA**:

Rejea katika Biblia yako, kwenye kitabu cha **Marko sura ya kumi na nne**, na tutasoma **mstari wa kwanza hadi kumi na moja**. Ni habari ya mwanamke aliyempaka Yesu mafuta huko Bethania (soma). **Mstari wa tisa** unasema: "*Ukweli nawaambieni, kila ihubiriwapo injili kote ulimwenguni, na hili aliloliifanya huyu litatajwa kwa kumbu-kumbu lake".* Na leo tunapotumia muda huu kusoma kifungu hiki; unabii huu wa Yesu unafanyika kuwa kweli! Kila mahali injili inapofundishwa, Yesu anasema, kutakuwa na nyakati ambapo wanaume na wanawake wataongelea juu ya kile ambacho mwanamke huyu alinifanyia mimi. Watakumbuka kujitolea kwake na sadaka yake. Alichokifanya hakitasahaulika. Na bila shaka Yesu anaposema hivi, anajua kwamba Mathayo, Marko, na Yohana wataijumuisha habari hii, wakati wanapoandika injili zao - ili ulimwengu wote uweze kusoma kuhusu hilo, kama vile tunavyofanya sasa. Luka pia anaandika habari ya kupakwa mafuta, lakini watu wengi wanafikiri kuwa habari hiyo siyo ile ile – ni mwanamke tofauti, na kwa wakati tofauti.

Kabla ya hatujangalia vitendo vya mwanamke huyu, napenda nitoe maoni juu ya kile kinachotokea katika **mstari wa kwanza na wa pili**. Mji wa Yerusalemu, kwa wakati huu, ulikuwa na shughuli nyingi. Kuna umati wa watu umekusanyika katika mji huu kutoka sehemu zote za Israeli – kwa lengo moja; la kusherehekea Pasaka pamoja na familia na marafiki zao. Ulikuwa ni wakati wa kutoa shukrani ili kukumbuka kutoka kwao **Misri**, na jinsi Mungu alivyo-waokoa mababu zao kutoka utumwani. Kipindi cha Pasaka kilikuwa ni kipindi cha kukumbuka, jinsi watoto wa Kiyahudi yaani wazaliwa wa kwanza walivyookolewa dhidi ya kifo, wakati huo wazaliwa wa kwanza wa Misri walikufa wote. Ilikuwa ni sherehe muhimu sana ya kukumbuka kwa watu wa Kiyahudi - na bado inaendelea hadi leo.

Tunaambiwa katika **mstari wa kwanza** kwamba, zilikuwa zimebaki siku mbili tu kuifikia sikukuu ya Pasaka. Makuhani na Walimu wa Sheria walikuwa wakitafuta kumkamata Yesu na kumwua. Lakini waliamua kutofanya hivyo wakati wa sikukuu ya Pasaka. Katika injili ya **Mathayo**, tunaambia kuwa katika hatua hii ya habari, Yesu anawaambia wanafunzi: "*Mwana wa Mtu atatiwa mkononi ili kusulubiwa*". Anawaambia wanafunzi wake kile kinachokaribia kutokea. Marko hakuyaaandika mazungumzo haya. Na tunajua kwamba kwa nyakati chache, Yesu alikuwa amemwambia wanafunzi wake kwamba angeuawa. Je, unakumbuka mara ya kwanza ambayo Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuhusiana na hili? Tayari tumeshaliangalia hili; katika **Marko sura ya nane**. Yesu aliwaambia kuwa angeteswa, na kukataliwa na Walimu wa Sheria, na ya kwamba wangemuua - lakini angefufuka tena kutoka kwa wafu baada ya siku **tatu**. Na katika tukio hilo, tunajua kuwa Petro alimkemea Yesu!

Ingawa Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi wake juu ya kifo chake angalau mara **tatu** hivi, wakati tunapofika katika **Marko sura ya kumi na nne**, wanafunzi bado hawaelewi kile ambacho Yesu alikuwa amekisema. Walikuwa hawako tayari kwa ajili ya kile kitakacho-tendeka katika Yerusalemu. Bila shaka wanajua kwamba viongozi wa dini hawakumpenda Yesu. Wanajua kwamba Yesu ana maadui, lakini hawakukubali kwamba Yesu anaenda kusulubiwa. Hawakuwa tayari. Lakini, katika kifungu chetu cha leo, tunamwona mtu mmoja ambaye alikielewa kile ambacho Yesu alikuwa akisema kuhusu kifo chake. Kuna mwanamke mmoja kutoka Bethania ambaye ni mfuasi wa Yesu, na pia ni rafiki wa Yesu. Yeye alikuwa ameaandaliwa tayari kwa ajili ya kifo chake. Yeye alikuwa amemsikiliza Yesu na alielewa kile alichokuwa amekisema. Na hivyo yeye anataka kuonyesha upendo wake kwa Yesu, kabla yeye hajauliwa.

Kabla ya kumwangalia mwanamke huyu na matendo yake, angalia kile kinachoendelea katika **mstari wa kwanza na pili**. Hapa tunawaona makuhani wakuu na Walimu wa Sheria wakipanga jinsi ya kumwua Yesu – lakini Yesu anajua zaidi kuhusu mipango yao kuliko walivyofanya. Anajua kile wanachokipanga kukifanya. Kwa kweli, Mungu ana udhibiti mchakato wote - na tunaweza kuona hayo katika **mstari wa pili**. Makuhani wakuu wamekubali kumkamata na kumuua Yesu - *"lakini sio wakati wa sikukuu, kwa sababu kunaweza kuwa na vurugu miongoni mwa watu".* Kwa hivyo walikuwa na mpango. Walikuwa wanakwenda kumkamata Yesu, lakini ni baada ya Pasaka. Lakini mipango hiyo ilibadilika haraka sana, wakati ambapo mmoja wa wanafunzi wa Yesu, alienda kwa makuhani wakuu na alikubali kumsaliti Yesu. Mipango yao ililazimika kubadilika.

Na hivyo walilazimishwa kumkamata Yesu. Unaona, Mungu alikuwa katika udhibiti wa matukio haya yote. Alikuwa hata katika udhibiti wa wakati ambao mwanawe angekufa.  Kifo cha Yesu ilibidi kitendeka siku ya Pasaka. Kwa nini? Kwa sababu Yesu alikuwa Mwana Kondoo wa Pasaka. Kumbuka habari ya Waisraeli katika kitabu cha **Kutoka**. Je, Waisraeli waliambiwa kufanya nini? Kuua mwanakondoo na kuweka damu yake juu ya milango ya nyumba zao - ili malaika wa kifo aweze kuzipita kwa kuruka nyumba zao, na bila kuua mzaliwa wao wa kwanza. Kwa njia hiyo hiyo, Yesu atauawa, na kwa sababu ya damu yake, kila mtu amwaminiye, atakuwa amefunikwa na damu yake, na hawezi kufa kiroho. Je, unaweza kuona jinsi kifo chake kinavyotukumbusha juu ya Pasaka, katika kitabu cha Kutoka? Yesu alitakiwa kufa wakati wao walipokuwa wakisherehekea Pasaka - kwa sababu alikuwa na utimilifu wa habari hiyo. Alikuwa Mwana Kondoo wa Pasaka ambaye angekufa kwa ajili ya dhambi za wengi.

Walikuwa wakipanga kumuua baadaye – lakini mipango yao ililazimika kubadilika. Na mipango yao ilibadilika, kwa sababu ya Yuda Iskariote - na tutayaona haya mwisho wa kifungu chetu, wakati Yuda alipoenda kwa makuhani ili kumsaliti Yesu. Kitu fulani kuhusu tukio hili katika Bethania, lilikuwa na athari kwa Yuda. Hakupenda kile kilichotokea hapa.

Ukisoma injili ya **Yohana**, utaona kwamba, kabla tu ya Pasaka, Yesu alikuwa akikaa katika kijiji cha Bethania. Hiki kilikuwa kijiji kidogo kama kilometa **mbili** hivi kutoka Yerusalemu, juu ya Mlima wa Mizeituni. Tunajua kwamba Lazaro na dada zake wawili, Mariamu na Martha waliishi huko - na Luka anatuambia pia kwamba nyumba yao ilikuwa wazi kwa ajili ya Yesu. Hivyo inawezekana kwamba, kwa wakati huu, Yesu huenda alikuwa akikaa nyumbani kwao. **Mstari wa tatu** wa kifungu chetu unatuambia kwamba, "*wakati alipokuwa Bethania*" alitembelea nyumba ya mtu aliyeitwa **Simoni Mkoma**. Kwa kweli, Simoni alikuwa amewaalika Yesu, na wanafunzi wake, kwa ajili ya chakula. Hatujui chochote kuhusu mtu huyu – isipokuwa kwamba jina lake lilikuwa Simoni, na jina lake la utani lilikuwa ni '*Mkoma*'. Hii sio jina nzuri sana kuwa nalo, sivyo?! Je, unaweza kufikiria kama utaitwa kwa jina la ugonjwa, ambao umekuwa ukiuugua!

Je, tunaijua nini kumhusu mtu huyu  aitwaye Simoni? Inawezekana kwamba alikuwa mtu maalumu, kutoka Bethania ambaye alikuwa akiteseka na ukoma - lakini Yesu alikuwa amemponya ugonjwa huo. Na Yesu alikuwa amealikwa nyumbani kwake ili kula chakula. Simoni anataka kumshukuru kwa kumwambia Yesu '*asante sana*', na hivyo yeye aliamua kumwalika aje nyumbani kwake kwa ajili ya chakula. Hii ni sherehe. Na kisha, katika **mstari wa tatu** unatuambia kwamba, mbele ya kila mtu katika sherehe, *"mwanamke alikuja kwake akiwa na chupa ya manukato, ambayo aliyamwaga juu ya kichwa cha Yesu.*' Bila shaka, watu walishitushwa; walishangazwa na kile ambacho mwanamke huyu alikuwa anakifanya.

Rejea katika kitabu cha **Yohana sura ya kumi na mbili** - na tutasoma **mstari wa kwanza hadi tatu**. Si Mathayo wala Marko anayetuambia jina la mwanamke huyo - lakini Yohana anatuambia jina lake. Simoni Mkoma, Yesu na wanafunzi wake, na pia Lazaro, na labda baadhi ya watu wachache kutoka kijijini pale, walikuwa wakifurahia chakula pamoja. Labda **Simon**i aliongelea kuhusu uponyaji wake, na labda watu walikuwa pia wakiuliza maswali kwa **Lazaro**, kwa sababu alikuwa amefufuka hivi karibuni kutoka kwa wafu! Yesu alikuwa ameamuru kwamba Lazaro apate uzima tena, hata kama alikuwa amekufa kwa siku **nne**. '*Tuambie jinsi ilivyokuwa Lazaro namna ya kurejea katika uzima yaani kufufuliwa*'. Watu Wanaongea na kufurahia chakula, wakati huo ghafla, Mariamu anamkaribia Yesu bila kutegemea.

Yeye anaifungua chupa, na kisha anayamimina manukato juu ya kichwa cha Yesu; na kisha, kama Yohana anavyosema katika injili yake, pia aliimina kiasi kwenye miguu yake. Na nyumba ilijawa na harufu nzuri.

Kwa hivyo, ni upi ulikuwa mwitikio wa wageni? Je, **Mstari wa nne** unasemaje? *"Baadhi ya wale waliokuwapo walikuwa wakisemezana wao kwa wao: kwa nini upotevu wa pesa. Ingeweza kuuzwa kwa mshahara wa mwaka, na fedha hiyo wangepewa maskini. Walikemea kwa ukali".* Kwa maneno mengine, baada ya kutambua jinsi manukato haya, yalivyokuwa kwa uthamani wake, waliudhika na walikasirika na kuudhika kwa kile ambacho Mariamu alikuwa amekifanya. Walifikiri huu ni upotezaji wa pesa. Watu hawa ni akina nani? Marko hataji majina yoyote hapa, lakini tunapoangalia katika injili ya Mathayo, anatuambia kwamba watu haya wailikuwa ni wanafunzi ndio, ambao walikuwa wamekasirishwa na Mariamu.

**Mathayo sura ya ishirini na sita, mstari wa nane** inasema: "*wanafunzi wake walipoona haya walikasirika*". Hata hivyo, kama ukiangalia katika injili ya Yohana, inatuambia kwamba alikuwa ni mmoja miongoni mwa wanafunzi, ambaye alikuwa na hasira. Mwanafunzi gani? **Yohana sura ya kumi na mbili, mstari wa arobaini na tano**: *"mmoja wa wanafunzi wake, Yuda Iskariote, ambaye baadaye alimsaliti, alipinga akisema; kwa nini mafuta haya hayakuuzwa na fedha wakapewa maskini? Na thamani ilikuwa ya mshahara wa mwaka mmoja".* Yuda hakuwa na furaha – lakini kwa nini? Naam, Yohana anatuambia kwa nini Yuda hakuwa na furaha katika mstari unaofuata: **Mstari wa sita**: *"hakuyasema haya kwa sababu ya kumjali maskini, lakini kwa sababu alikuwa ni mwizi".* Yohana pia anatuambia kwamba Yuda alikuwa ni mtu ambaye alikuwa akitunza fedha za wanafunzi – na kwamba aliendelea kuiba kutoka akaunti hiyo. Tatizo la Yuda ni kwamba yeye alikuwa mwizi, ambaye alikuwa na tamaa ya fedha - na hii inatusaidia kuelewa kwa nini alitaka kumsaliti Yesu. Yeye alitaka apate vipande **thelathini** vya fedha.

Je, unaweza ufikiria namna unavyoweza kujisikia kuwa katika chumba hicho, wakati jambo hili lilipotokea? Hapa yupo huyu mwanamke Mariamu, ambaye alikuwa amemimina mafuta yake, juu ya miguu na kichwa cha Yesu, na wanafunzi wakimkemea. Walikuwa na hasira naye kwa kufanya kitendo hicho, hii ni kwa sababu walifikiri angeweza kuitumia fedha hiyo kwa njia bora zaidi. Kwa nini walikuwa walikuwa wakiwajali maskini? Kwa upande mmoja, ni vizuri kwamba wanafunzi walikuwa wakionesha kuwajali maskini - na labda moja ya sababu ya kuwajali ilikuwa ni Pasaka wakati, ambapo waliwakumbuka maskini. Kwa kweli, ilikuwa desturi, jioni kabla ya Pasaka, kwamba watu wangetoa zawadi za fedha, na chakula, kwa maskini. Hii inasaidia kuelezea maoni, ambayo Yohana anayatoa katika injili yake, kuhusu usaliti wa Yuda. Je, unakumbuka wakati Yesu na wanafunzi wakiwa katika chumba cha juu, na Yesu akamwambia Yuda, *"kile ambacho unakaribia kukifanya, nenda na ukifanye haraka*". Naam,

Yohana anasema haya katika injili yake kwamba, hakuna hata mmoja wa wanafunzi aliyeelewa kwa nini Yesu alikuwa akimwambia hivyo. Hawakuweza kulielewa. Katika **Yohana sura ya kumi na tatu, mstari wa ishirini na tisa** tunaambiwa: *"kwa kuwa Yuda alikuwa akitunza fedha, baadhi ya wanafunzi walidhani kwamba Yesu alikuwa anamwambia Yuda, akanunue kile wanachokihitaji kwa ajili ya sikukuu, au **kutoa kitu kwa maskini**".* Nafikiri aya hiyo inaleta maana kubwa, wakati tunapotambua kwamba ilikuwa desturi katika pasaka kuwaangalia maskini, na labda hii ni sababu ambayo wanaifikiria juu ya maskini, baada ya kumwona Mariamu akimwaga manukato ya ghali sana. Na kwa hivyo wakamkemea kwa kufanya hivyo.

Na kisha katika **mstari wa sita** tumefika katika hatua au pointi kuu ya kifungu. Yesu anajua kile ambacho wanafunzi wanakisema, na anaingilia kati kumlinda Mariamu. Yesu anawakemea wanafunzi, na kuwaambia: *“Muacheni peke yake. Kwa nini mnamsumbua? Amenifanyia jambo zuri mimi".* **Mstari wa saba**: "*maskini mtakuwa nao daima na, na mnaweza kuwasaidia wakati wowote mnaotaka - lakini mimi hamko nami daima".* **Mstari wa nane:** "*ametenda alivyoweza; amegangulia kuupaka mwili wangu marhamu kwa kuniandaa kwa maziko yangu".* Kwa maneno mengine, kile ambacho Mariamu amefanya kwangu, ni kitendo cha upendo na ibada. Amenipa mali yake ya thamani. Amefanya kitu kizuri kwangu. Na hii hapa ni changamoto kwetu - wakati Yesu anapotutazama, na kutuona jinsi tunavyoishi, Je, anaona kitu kizuri, au kitu kibaya? Je, yeye huiona ibada yetu kwake? Je, hutuona sisi tukitoa muda wetu ,na fedha zetu kwake katika njia ya kafara? Je, tunafanya huduma nzuri kwa Yesu? Je, tunampa yale yaliyo bora katika maisha yetu?

Angalia tena katika **mstari wa tano** jinsi manukato haya yalivyokuwa ya thamani.  Marko anatuambia kwamba kama yangeweza kuuzwa manukato ni zaidi ya mshahara wa mwaka mmoja! Katika injili ya Yohana tunaambiwa kwamba Mariamu alitumia nusu lita ya **marhamu ya Nardo safi**. Hii ilikuwa ni marhamu maalum, inayochukuliwa kutoka katika mimea, ambayo hukuzwa huko **India**. Na Mtume Yohana anataka tujue kuwa ilikuwa ghali sana. Ni gharama kubwa ya fedha. Manukato haya yalikuwa na thamani kiasi gani? **Mstari wa tano** wa kifungu chetu, unatuambia kuwa ilikuwa ni ya thamani zaidi ya mshahara wa mwaka. Kama ungekuwa unasoma habari hii katika lugha ya Kigiriki, ungeweza kusema kwamba ilikuwa na thamani ya **dinari mia tatu.** Hiyo haina maana yoyote kwetu leo, hivyo basi ngoja nijaribu kuelezea.

Katika siku hizo, **miaka elfu mbili** iliyopita, kama ungekuwa kibarua, mshahara wa siku moja ulikuwa **dinari moja**. Hivyo, kama ulifanyakazi kwa mwaka mmoja, kwa **siku sita** kwa wiki, unaweza kupata **dinari mia tatu**. Katika Tanzania, labda kibarua anapata kulipwa **shilingi elfu nane**, labda zaidi, labda chini ya hapo. Lakini kama alilipwa **shilingi elfu nane** kwa kila siku, kwa **siku sita** kwa wiki, angeweza kulipwa **milioni moja, laki mbili**. Hiyo ni fedha nyingi. Lakini kumbuka, Mariamu hakuwa kibarua. Pengine hakuwa na hata kazi,  hivyo manukato haya yalikuwa ni ya thamani sana kwake. Pengine ni kitu cha thamani sana ambacho yeye alikuwa akikimiliki. Yeye anaivunja, na kumimina marashi juu ya miguu ya Yesu. Ni dhabihu kubwa sana kwake. Wanafunzi hawaelewi hili, na kwa hiyo wanakemea,  lakini Yesu anajua ni kwa nini amefanya hivyo, naye anakikubali kile alichokifanya. "*Mariamu amefanya kitu kizuri kwangu*".

Hapa kuna swali tena. Je, tuko tayari kumpa Mungu kile ambacho ni cha thamani zaidi kwetu? Je, tuko tayari kutoa maisha yetu kwa Yesu? Je, tuko tayari kumwambia Mungu, chukua vyote vya kwangu. Au Je, hatuna uhiari wa kumwachia kila kitu? Je, kujitoa kwako kwa Yesu kunagharimu chochote? Miaka michache iliyopita nilisikia hadithi kutoka Afrika Magharibi.

*"Kulikuwa na mkulima mdogo mwanamke, ambaye aliishi kijijini pamoja na familia yake. Siku moja akawa Mkristo na alitoa maisha yake kwa Mungu. Alikuwa na shukrani sana kwa kuwa Mungu alikuwa ameokoa, na kumtoa kutoka katika maisha yake ya dhambi. Imani yake ilikuwa hai ingawa alikuwa maskini. Siku moja, kulikuwa na mkutano mkubwa katika kijiji, na baadhi ya wainjilisti walikuja kuhubiri injili. Wakati wa ibada, kulikuwa na matoleo, na baadhi ya watu walikuwa wakionekana wakileta zawadi za mahindi, badala ya fedha. Lakini mwanamke huyu alikuwa maskini sana, na hakuwa na kitu cha kutoa. Hata hivyo, wiki moja baadaye kulikuwa na ibada nyingine, na wakati huu katika ibada, alienda mbele ya Kanisa, na akatoa **sarafu moja** ya dhahabu. Ilikuwa ni ya thamani sana.*

*Mchungaji alishangazwa kumwona akitoa sana, kwa sababu alijua kuwa alikuwa maskini sana. Baada ya ibada alikwenda kuzungumza naye, na kumuuliza alikuwa ameipata wapi sarafu ya dhahabu. Mwanamke alisema kwamba, kwa sababu Mungu alikuwa amemweka huru kutoka katika dhambi zake, na alikuwa amempa uzima wa milele, alitaka kumtumikia, na kufanya kitu ili kuonyesha kujitoa kwake. Hivyo alikuwa amekwenda shambani, na kujiuza mwenyewe kwa m-miliki kama mtumwa kwa ajili ya maisha, kwa ajili ya sarafu moja ya dhahabu – na ya kwamba hii ilikuwa ni zawadi yake aliyoitoa Kanisani usiku ule".* Aliyauza maisha yake na kuitoa fedha ile Kanisani – hata hivyo alitakiwa kufanya kazi shambani kwa maisha yake yote. Aisee! Hiyo ndiyo ibada! Je, **Warumi sura ya kumi na mbili, mstari wa kwanza** inasema nini?

"*Nawasihi, kwa huruma yake Mungu, kwa sababu ya kile alichokifanya kwa ajili yenu, itoeni miili yenu kuwa dhabihu hai, takatifu na ya kupendeza kwa Mungu, kwa hili ni tendo lenu la kiroho la ibada".* Toeni maisha yenu kwa ajili yake, na kwa ufalme wake.

Pamoja na hayo, baini kwamba Mariamu alitoa kitu cha thamani sana – kwa namna ile ile Yesu naye, alikuwa karibu kutoa kitu cha thamani kubwa sana. Kama vile Mariamu anavyo-mimina manukato ya thamani, kama zawadi kwa Yesu – kwa njia hiyo hiyo, Yesu anajiandaa kumwaga damu yake msalabani. Mariamu akamwaga mafuta, na hakubaki na chochote kwa ajili yake mwenyewe. Alitoa vyote kwa Yesu. Kwa njia hiyo hiyo, Yesu yuko karibu kuyatoa maisha yake, kwa kujisalimisha kikamilifu, kama ishara ya upendo wake na kujitoa kwa Mungu Baba, na kwetu sisi.

Lakini pia kuna kitu kingine ambacho Yesu alipongeza Mariamu kwa ajili yake. Kumbuka mwanzoni mwa kipindi hiki, nilieleza kwamba wanafunzi hawakuelewa kwamba Yesu alikuwa anaenda kufa – lakini kulikuwa na mtu mmoja ambaye alielewa kile ambacho Yesu alikuwa akikisema. Angalia **mstari wa nane**: "*yeye amemwaga manukato juu ya mwili wangu kwa kujiandaa kwa ajili ya mazishi yangu".* Mariamu alielewa mafundisho ya Yesu, na alijua kile kitakachotokea kwake. Na hivyo aliamua kumwonyesha Yesu jinsi alikuwa ni mwenye shukrani; aliamua kumwonyesha Yesu kwamba yeye alijitoa kwake, wakati bado kulikuwa na wakati, kabla ya kufa. Hakuwa na wasiwasi juu ya vile watu wengine watakavyomfikiria. Hakuji-shughulisha na wala hakuwa wasiwasi kuwa baadhi ya watu wangemkema. Hakujali kile wengine walichomwambia. Kumbuka, katika injili ya Yohana, tunaambiwa kwamba yeye alimwaga pia manukato juu ya miguu ya Yesu, na kisha akaisafishwa kwa nywele zake. Hiyo ina maana kwamba yeye lazima alikuwa na nywele ndefu - na katika siku hizo, kama wewe ungekuwa ni mwanamke, haikukubalika kuwa na nywele ndefu katika umma. Ni lazima uzifunge. Lakini hapa tunamwona Mariamu, katika sherehe, na yeye anatumia nywele zake kuifuta miguu ya Yesu. Yeye alipiga magoti, kama mtumwa mnyenyekevu, akiifuta miguu ya mabwana zake, kwa nywele zake. Na hakujali kile wengine walichofikiria juu yake. Alitaka kumpaka mafuta Yesu wakati wa

mlo huu, kwa sababu alijua kwamba inaweza kuwa ni mara ya mwisho, ambao angeweza kuonyesha hali ya kujitoa kwake - na Yesu alimsifa kwa ufahamu wake.

Pamoja na hayo, neno '*Masihi*' lina maana ya '*mpakwa mafuta*'. Fikiria kuhusu hili. Hapa ni Mariamu anayempaka mafuta '*mpakwa mafuta*' - katika njia ile ile ambayo wafalme wa Agano la Kale, walikuwa wakitiwa mafuta. Wakati mfalme alipoanza utawala wake, alipakwa mafuta kichwani pake, lakini kwa Yesu, badala ya kupakwa mafuta mwanzoni mwa utawala wake, alipakwa mafuta kama mfalme mwishoni mwa maisha yake na mwanamke aliyeitwa Mariamu, ambaye alitaka kuonyesha upendo wake.

Tunajua pia kwamba Mariamu alijua kuwa Yesu alikuwa anaenda kufa, kwa sababu ya aina manukato aliyoyachagua. Manukato haya, au mafuta, yaliitwa nardo - na haya mara nyingi yalitumika kwa ajili ya kupaka maiti. Yalikuwa ni manukato yaliyounganishwa na kifo. Kumbuka, katika siku hizo, miili haikuzikwa chini ya ardhi kama ilivyo leo. Mtu alipokufa, mwili ungeweza kuchukuliwa kwenye kaburi, au pango, na ulipakwa manukato na mafuta, na kisha huviringishwa kwenye nguo. Na hii ilifanyika ili kuzuia harufu mbaya ya mwili ulioza. Baada ya mwili kupakwa mafuta, kaburi lilikuwa likifunikwa kwa jiwe kubwa. Wakati Mariamu alipochagua manukato, alijua kuwa Yesu alikuwa anaenda kufa, na hivyo alitaka kuonyesha upendo wake, kabla ya hajafa.

Tunapofika katika **mstari wa tisa** tunaona kwamba Yesu alivutiwa na kile ambacho Mariamu alikuwa amekifanya, anasema hivi: "*nawaambia ukweli, popote injili hii itakapohubiriwa kote ulimwenguni, kile ambacho amekifanya pia kitasemwa, kwa kumbukumbu lake".* Habari yake imekuwa sehemu ya injili; imekuwa sehemu ya habari njema. Je, kuna somo gani hapa? Yesu anataka kile kilichochema kutoka kwetu. Anatutaka tumpe maisha yetu. Anatutaka sisi kumweka Yeye kuwa wa kwanza zaidi ya kitu kingine chochote, hata kama tuko maskini. Yesu anatutaka sisi kutoa maisha yetu ya thamani kwake kama sadaka. Lakini kwa huzuni, kifungu chetu kinaishia katika mstari wenye huzuni sana. Tumekiona kile ambacho Mariamu alikifanya. Ni habari kubwa kuhusu mtu akimwonyesha Yesu upendo. Lakini halafu, tuna habari iliyo kinyume katika **mstari wa kumi na kumi na moja**. Tuna habari ya mtu ambaye alikuwa mchoyo na tamaa ya fedha, na akaamua kumsaliti Yesu. *"Ndipo Yuda Iskariote, mmoja wa wale thenashara, alikwenda kwa Makuhani Wakuu ili kumsaliti Yesu. Walifurahia kusikia hili na kuahidi kumpa fedha. Na hivyo aliangalia nafasi ya kumtoa".* Na hivyo kifungu kinaisha kwa huzuni, sio kwa furaha.

Hii ni habari ya mwanamke mmoja, ambaye alikuwa amejitoa kwa Yesu – na habari ya mtu mmoja aliyemsaliti Yesu. Mariamu alitoa kitu muhimu sana kwa Yesu. Hakujali manukato yalikuwa na thamani gani, alitaka kumpaka Yesu mafuta. Lakini hapa pia kuna Yuda, ambaye hataki kutoa chochote kwa Yesu, lakini badala yake anataka kupata fedha kwa kuuza Yesu kwa makuhani. Mariamu alitoa kitu ambacho kilikuwa cha thamani ya mshahara wa mwaka mzima - **dinari mia tatu**. Yuda angemsaliti Yesu kwa sarafu **thelathini** za fedha – hiyo ni sawa na **dinari mia moja, na ishirini**. Hii ni habari nzuri ya mwanamke mmoja ambaye alitaka kutoa, na habari mbaya ya mtu mmoja ambaye alitaka kuchukua. Mariamu alitoa, Yuda alichukua. Mariamu akatoa kwa ukarimu kuonyesha upendo wake. Yuda alichukua fedha kuonyesha kwamba yeye hana upendo na Yesu. Na tunajua kwamba ili-isha vibaya sana kwake. Je, wewe ni mchungaji au mwinjilisti ambaye unataka kutoa kwa Yesu – au kuchukua kutoka kwake? Je, tuko tayari kuonyesha upendo wetu kwa Yesu, au je matendo yetu yanaonyesha kwamba tunamsaliti Yesu?

-----------------------------------------------